Barry, A. L. - WHAT ABOUT? BEING A LUTHERAN - Swahili

Kuhusu Jambo Gani...

# Kuwa Mlutheri

**Daktari A. L. Barry**
**Rais**
**Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri**

## Hakika, Mlutheri ni Nani?

Ingawa kuna njia nyingi za kulijibu swali hili, jibu moja muhimu sana hasa ni hili, "Mluthheri ni mtu aaminiye, afundishaye, na akiriye kweli za Neno la Mungu kama zinavyofupishwa na kukiriwa katika Kitabu cha Mwafaka." Kitabu hiki kina Kiri za Imani ya Kilutheri.

Labda umehudhuria sherehe ya anayebarikiwa kuwa mchungaji na kumsikia akiahidi kwamba, atatekeleza wajibu wa afisi yake kufuatana na Kiri za Kilutheri. Watu wanapopokea kipaimara, wanaulizwa kama wanalikiri fundisho la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri, kama walivyokwisha kujifunza kutoka kwa Katekisimo Ndogo, kuwa waaminifu na wakweli.

Ahadi hizi za heshima hutuonyesha jinsi Kiri za kilutheri zilivyo muhimu kwa kanisa letu. Hebu tuvichunguze vipengele mbalimbali katika Kitabu cha Mwafaka na kisha tutazungumzia ni kwa nini Kiri za Kilutheri ni muhimu sana kwa mtu kuwa Mlutheri.

## Kiri Tatu za Kiekumeni ni Zipi?

Kiri tatu za kiekumeni katika Kitabu cha Mwafaka ni Ukiri wa Mitume, Ukiri wa Nikea, na Ukiri wa Athanasio. Zinaelezewa kama za kiekumeni (za Wakristo wote ulimwenguni) kwa sababu zinakubaliwa na Wakristo ulimwenguni kote kama semi sahihi za yale yafundishwayo na Neno la Mungu.

## Ni Nini Ukiri wa Augsburg na Utetezi wa Ukiri wa Augsburg?

Mwaka wa 1530, Walutheri walihitajika kuwasilisha ukiri wao wa imani mbele ya kaisari huko Augsburg, Ujerumani. Filipo Melanchthon ndiye aliyeandika Ukiri wa Augsburg na ulisomwa mbele ya mahakama kuu tarehe 30 Juni, mwaka wa 1530. Mwaka mmoja baadaye, Walutheri walitoa utetezi wao wa Ukiri wa Augsburg, ambao maana yake hapa ni "utetezi." Utetezi huu pia uliandikwa na Filipo Melanchthon. Ndilo andiko [Utetezi] refu sana katika Kitabu cha Mwafaka, sura ndefu sana, inayotengwa kwa kweli muhimu sana ya imani ya Kikristo: fundisho la kuhesabiwa haki kwa neema pekee, kwa njia ya imani pekee, na katika Kristo pekee.

## Ni Nini Katekisimo Ndogo na Katekisimo Kubwa?

Martin Luther alitambua mapema namna Wakristo wa kawaida na wachungaji wa wakati wake walikosa kujua hata kweli za kimsingi sana za imani ya Kikristo. Mnamo mwaka wa 1530, alitoa vijitabu viwili vya maelekezo ili kuwasaidia wachungaji na wakuu wa familia wafundishe imani.

Katekisimo Ndogo na Katekisimo Kubwa vi juu ya mada (topics) sita: Amri Kumi, Ukiri wa Mitume, Sala ya Bwana, Ubatizo Mtakatifu, Ukiri, na Sakaramenti ya Madhabahu. Mihtasari hii bora ya mafundisho iliyoandikwa na Luther ilikubalika ulimwenguni kote, kiasi kwamba, iliingizwa kuwa sehemu ya Kitabu cha Mwafaka.

## Ni Nini Mafungu ya Smalkaldi na Makala Kuhusu Mamlaka na Ukuu wa Papa?

Mwaka wa 1537, Martin Luther aliulizwa kutayarisha hoja ya imani ya Kilutheri ili itumike katika baraza la kanisa, iwapo lingeitwa [baraza]. Ukiri jasiri na wa juhudi wa imani ulioandikwa na Luther uliingizwa baadaye katika Kitabu cha Mwafaka. Uliwasilishwa katika mkutano wa kundi la watawala Walutheri mjini Smalkaldi. Filipo Melanchthon aliombwa kufafanua juu ya papa wa Roma na alifanya hivyo katika makala yake, ambayo pia yaliingizwa katika Kitabu cha Mwafaka.

## Ni Nini Shauri la Mwafaka?

Baada ya kifo cha Luther kilichotokea mwaka wa 1546, mabishano makuu yalizuka katika Kanisa la Kilutheri. Baada ya majadiliano na kushindana kwingi, Shauri la Mwafaka lilikomesha mabishano haya ya mafundisho mwaka wa 1577 na Kanisa la

Kilutheri liliweza kuendelea likiwa moja katika yale lililoyaamini, lililoyafundisha, na lililoyakiri. Mwaka wa 1580, maandiko yote ya kiukiri yanayotajwa humu yalikusanywa katika juzuu moja, yaani, Kitabu cha Mwafaka. Mwafaka ni neno lenye maana ya "mapatano."

**Kuna Uhusiano Gani Kati ya Biblia na Kiri?**

Tunakiri kwamba, "Neno la Mungu halina budi kubaki kama kaida na kanuni kamili ya mafundisho yote" (SM TT, Kaida na Kanuni, 9). Lisemwalo na Biblia, ndilo Mungu hulisema. Liamriwalo na Biblia, ndilo Mungu huliamuru. Mamlaka ya Maandiko Matakatifu ni makamilifu, hakika na mwisho. Kiri za Kilutheri zinayakubali Maandiko Matakatifu kama Neno la Mungu halisi. Kiri za Kilutheri hutuhimiza kuamini Maandiko Matakatifu maana "hayatadanganya" (KK, V, 76) na hayawezi kuwa "uongo wala hayadanganyi" (SM TT, VII, 96). Biblia ni "Neno la Mungu lililo safi, lisilokosea, na lisilobadilika" (Dibaji ya Kitabu cha Mwafaka).

Kiri za Kilutheri ndizo "msingi, kaida, na kanuni inayoonyesha namna maandiko yote yanapaswa kuchunguzwa na kupimwa kufuatana na Neno la Mungu" (SM TT, KAIDA NA KANUNI). Kwa kuwa Kiri zinafuatana na mafundisho kamili ya Neno la Mungu lililoandikwa, zinafanya kazi kama usanifu katika Kanisa la Kilutheri ili kuonyesha ni lipi lililo fundisho aminifu la Kibiblia, kwa mujibu wa jinsi fundisho linavyofafanuliwa katika Kiri.

**Lipi ndilo Jambo Kuu la Kiri za Kilutheri?**

Matengenezo ya Kilutheri hayakuwa "maasi," bali yalianza kama maelezo ya shughuli ya kweli juu ya mafundisho ya uongo na mapotovu, ambayo, kwa bahati mbaya, mpaka hata sasa, husitiri utukufu na stahili ya Yesu Kristo. Kilichomvutia Luther ni bidii ya kuishughulikia Injili ya Yesu Kristo. Hapa, Kiri za Kilutheri huelezea ni nini kazi ya Injili:

"Wanadamu hawajaishika sheria ya Mungu bali wameivunja. Asili yao ya kibinadamu inayoharibu, kwa mawazo, kwa maneno, na kwa matendo yao hushindana na sheria. Kwa sababu hiyo, wako chini ya ghadhabu ya Mungu, ya mauti pamoja na ya mateso yote ya dunia hii, na adhabu ya moto wa jehanum. Mwisho wake, Injili, katika ukali wake, hufundisha yanayowapasa kuyaamini watu, yaani, kwamba, wamepokea msamaha wa dhambi kutoka kwa Mungu; kwamba, Mwana wa Mungu, Kristo Bwana wetu, Yeye Mwenyewe ametuchukulia laana ya sheria, amepatanisha na kufidia dhambi zetu zote; kwamba, kwa njia Yake pekee tumerejeshwa kwa neema ya Mungu, tumepokea msamaha wa dhambi kwa njia ya imani na tumekombolewa kutoka mautini na kutoka kwa adhabu zote za dhambi zetu na tunaokolewa milele . . . Ndizo habari njema, za furaha, kwamba, Mungu hapendi kuiadhibu dhambi bali anataka kuisamehe kwa ajili ya Kristo" (SM TT, V, 20).

**Ni Nani Mlutheri Mwenye Kukiri?**

Neno "ukiri" linatumika kwa njia mbalimbali, lakini tunapozungumzia kuhusu Mlutheri "mwenye Kukiri," tunamaanisha Mlutheri ambaye huutangazia ulimwengu imani yake na ayaaminiyo sana moyoni kwa uthibitifu (conviction), wa kupatana na maandiko yapatikanayo katika Kitabu cha Mwafaka. Katika haya, utapokea roho yenye kukiri ya Ulutheri, maneno ya mwisho yaliyoandikwa katika Kitabu cha Mwafaka:

"Kwa hiyo, mbele za Mungu na mbele ya Wakristo wote wa sasa na vizazi vyetu vijavyo, tungependa kushuhudia kwamba, maelezo haya ya mafungu yaliyojadiliwa na kuelezewa awali, yanalingana kabisa na mafundisho, imani, na ukiri wetu. Kwa neema ya Mungu, tunataka kuonekana mbele ya kiti cha hukumu cha Yesu Kristo, kuwa wenye mioyo thabiti na kuitoa hesabu yake. Sisi hatutaki kusema na kuandika kinyume chake, kwa siri wala hadharani. Badala yake, kwa

neema ya Mungu, tunakusudia kuyazingatia." (SM TT, XII, 40).

**Ni Nini Kukubali kwa Kiri Zisizokuwa na Masharti?**

Wachungaji Walutheri wenye Kukiri wanahitajika "kukubali" Kiri za Kilutheri bila masharti kwa sababu wao ni ufafanuzi safi wa Neno la Mungu. Hii ndiyo njia wachungaji wetu, pamoja na kila Mkristo wa kawaida ambaye hukiri imani yake katika Katekisimo Ndogo, anaweza kusema kile anachokiamini kuwa kweli ya Neno la Mungu kwa furaha kuu na bila shaka au bila kikwazo.

Daktari C. F. W. Walther, Rais wa kwanza wa Sinodi ya Missouri, alielezea maana ya kukubali kwa ukiri usiokuwa na masharti katika maneno yaliyo wazi na makali siku hizi sawa na yalivyokuwa wakati huo:

"Kukubali kusikokuwa na masharti ndilo tangazo la pekee ambalo mtu atakaye kulihudumia kanisa hutoa katika kiapo kwamba, anakubaliana na yaliyomo ya fundisho la Kiri zetu za Kilutheri, kwa sababu hutambua ukweli kwamba, linapatana kabisa na Maandiko Matakatifu na halizuii Maandiko Matakatifu katika jambo lolote, liwe ndogo au kubwa; na kwamba, kwa sababu hiyo, huamini kwa moyo wake wote katika kweli hii ya Kimuungu na anajitolea kulihubiri fundisho hili."

**Kwa hiyo, ni Nini Kuwa Mlutheri?**

Kuwa Mlutheri ni kuwa mtu anayeamini kweli za Neno la Mungu, Biblia Takatifu, kama vyenye kuelezewa kwa usahihi na kufundishwa katika Kitabu cha Mwafaka. Kutenda hivyo ni kuikiri Injili ya Yesu Kristo. Walutheri wa kweli, Walutheri wa kukiri, huthubutu kusisitiza kwamba, "Mafundisho yote lazima yalingane na vipimo vilivyowekwa hapo juu. Lolote lililo kinyume cha hayo lazima likataliwe na lilaaniwe ikiwa linapingana na azimio la pamoja la imani yetu inayokubaliwa na wote" (SM Mh. KAIDA NA KANUNI, 6).

Kwa wengine, kauli kama hiyo inaweza kuonekana kama yenye majivuno. Lakini sivyo; badala yake, ni usemi wa tumaini linaloongozwa na Roho anayetusukuma tuitaje imani yetu mbele ya ulimwengu.

Kuwa Mlutheri wa kukiri ni kuwa anayeliheshimu Neno la Mungu. Neno hilo linadhihirisha kwamba, ni mapenzi ya Mungu kwa kanisa Lake kupatana na mafundisho, na kuwa na nia moja, likikaa katika amani (1 Kor. 1:10; 2 Kor. 13:11). Ni kwa sababu hii tunathamini ukiri wenye thamani wa kweli ya Kikristo tulio nao katika Kitabu cha Mwafaka. Kwa Walutheri wa kukiri, hakuna kusanyiko jingine la maandiko, au kauli au vitabu ambavyo huwasilisha mafundisho ya Neno la Mungu na huifunua Injili ya Biblia dhahiri, sawasawa na kwa kufariji sana kuliko Kitabu cha Mwafaka.

Pamoja na kujitolea kwetu kwa mafundisho safi na ukiri wa imani, ni, na lazima tujitolee kuuendea ulimwengu kwa njia ya Injili na kuiambia kweli ya Mungu kwa ujasiri. Katika uchunguzi wa mwisho, hiyo ndiyo maana ya "ukiri" wa imani. Naam, "Kama ilivyoandikwa: 'Naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena.'" (2 Kor.4:13). Hii ndiyo maana ya kuwa Mlutheri.

**Tanbihi:**

**SM**: Shauri la Mwafaka

**TT**: Tamko Thabiti

**KK**: Katekisomo Kubwa

**Kaida na Kanuni**: Rule and Norn

**Muh.**: Muhtasari

Daktari A. L. Barry
Rais
Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri